# JARIDA LA DODOJI

"Let's Us Share the Gift of Nature Together"

Julai - Disemba, 2025 Toleo Na. 04



**NI JUKUMU LA KILA MTANZANIA KULINDA RASILIMALI ZA UVUVI- DKT. BASHIRU**

...................... UK. 01

HALIUZWI

# YALIYOMO

## MARINE PARKS AND RESERVES TANZANIA (MPRU)

S.L.P 7565, DAR ES SALAAM
+255 222150621
marineparks@marineparks.go.tz
www.marineparks.go.tz

01 NI JUKUMU LAKILA MTANZANIA KULINDA RASILIMALI ZA UVUVI - DKT. BASHIRU

02 NAIBU KATIBU MKUU, OR - KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI ZANZIBAR ASISITIZA UMUHIMU WA KUTUNZA MIAMBA YA MATUMBAWE KWA KUWA INACHANGIA UKUAJI WA UCHUMI NCHINI

03 MPRU YASHIRIKI SEMINA YA MKAKATI WA KITAIFA WA KUSIMAMIA NA KUENDELEZA MISITU YA MIKOKO

04 MPRU YASHIRIKI MAONESHO YA KIMATAIFA YA KIBIASHARA YA 49 SABASABA 2025

05 MPRU YASHIRIKI SEMINA YA KIMATAIFA YA MAENDELEO NA USIMAMIZI WA UCHUMI WA BAHARI NCHINI CHINA

06 MKUU WA WILAYA YA MTWARA AZINDUA RASMI TAMASHA LA NYANGUMI 2025

07 TUSIHUJUMU VIUMBE WA BAHARINI KWA UVUVI HARAMU NA TAKA NGUMU - DC MTWARA

08 WAHIFADHI BAHARI, WANAJAMII WA MAFIA WAHITIMISHA MAFUNZO YA UKUFUNZI WA UREJESHWAJI WA MATUMBAWE NCHINI INDONESIA

09 WATANZANIA WAPATIWA FURSA YA KUJIFUNZA KIDIJITALI JUU YA UHIFADHI WA MATUMBAWE

10 USAFI WA KISIWA CHA JAMBE KUFUNGUA MILANGO YA UTALII TACMP

11 MPRU WARSHA YA KUHUISHA MPANGO WA JUMLA WA UHIFADHI DMRS

12 WATUMISHI WATATU (3) MPRU-TMRS WAPATIWA MAFUNZO YA UREJESHWAJI WA MIAMBA YA MATUMBAWE

13 MPRU NA WANAJAMII MAFIA WASHIRIKI MAFUNZO YA UREJESHWAJI WA MIAMBA YA MATUMBAWE NCHINI INDONESIA

14 MPRU YAFIKIA WANANCHI KWA WINGI KATIKA MAONESHO YA NANENANE MKOANI LINDI

15 MPRU YAELEZA UMUHIMU WA UHIFADHI WA BAHARI KATIKA KUKUZA UCHUMI WA BULUU








# NI JUKUMU LA KILA MTANZANIA KULINDA RASILIMALI ZA UVUVI-DKT. BASHIRU

Na **Arafat Mnyau**

Haziri wa Mifugo na Uvuvi B Mhe. Bashiru Ally Kakurwa amepiga marufuku matumizi ya maneno "Uvuvi haramu" ambapo badala yake ametaka vitendo hivyo sasa vitambulike kama Uvuvi usiozingatia sheria na watu wanaofanya hivyo watambulike kama wahalifu.

Mhe. Balozi Dkt. Bashiru ameyasema hayo wakati akizungumza na watendaji na watumishi wa kitengo cha Uhifadhi wa Maeneo Tengefu alipofika kukagua utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kitengo hicho Disemba 06,2025 jijini Dar es Salaam.

"Hakuna Uvuvi haramu, suala la uharamu na uhalali ni suala la Mwenyezi Mungu sasa mtu haramu maana yake aende motoni na sisi hapa duniani na Serikalini hatuna moto wa kupeleka watu wanaovua uvuvi haramu" Amesisitiza Mhe. Balozi Dkt. Bashiru

Mhe. Balozi Dkt. Bashiru ameongeza kuwa vitendo vya



Uvuvi usiozingatia sheria vinatokana na kukosekana kwa utawala wa sheria katika sekta ya Uvuvi suala ambalo amesisitiza kuwa linapaswa kutekelezwa na kila Mtanzania.

"Kwa hiyo mimi sitakuwa na msamiati wa Uvuvi haramu kwa sababu Rais hajateua masheikh, mapadri, wachungaji au mitume bali ameteua Watanzania

Aidha Mhe. Balozi Dkt. Bashiru ametoa kwa Watanzania popote walipo pindi wanaposhuhudia vitendo vinavyoashiria Uvuvi usiozingatia sheria wahakikishe wanawachukulia hatua za kisheria watu hao.kusimamia sheria na kama sheria ni dhaifu bunge lipo na mimi ndo ninaiwakilisha sekta ya Uvuvi na Mifugo bungeni kwa hiyo tuimarishe sheria zetu" alisema Mhe. Balozi Dkt. Bashiru

# NAIBU KATIBU MKUU, OR-KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI ZANZIBAR ASISITIZA UMUHIMU WA KUTUNZA MIAMBA YA MATUMBAWE KWA KUWA INACHANGIA UKUAJI WA UCHUMI NCHINI




Na **Arafat Mnyau**

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwekezaji Zanzibar, Dkt. Rashid Ali Salim amesisitiza umuhimu wa kulinda miamba ya matumbawe kwa kuwa inachangia ukuaji wa uchumi wa nchi kwa kuvutia watalii kutoka kote duniani.

Aliyasema hayo Julai 22, 2025 wakati wa uzinduzi wa Mpango wa Kitaifa wa Uhifadhi wa Miamba ya Matumbawe Imara (NAPCRCR) uliofanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano katika Hoteli ya Peacock iliyopo jijini Dar es Salaam na kueleza matarajio yake kuwa utekelezaji wa mpango huo utatatua changamoto mbalimbali zinazokumba Hifadhi za Bahari, ikiwemo uvuvi haramu, mabadiliko ya tabianchi pamoja na uharibifu wa mazingira.

"Ingawa nchi inanufaika sana kupitia utalii mkubwa, ustawi wa kiikolojia, usalama wa chakula, biashara, uwekezaji, na ustawi wa jamii za pwani, ili tuweze kufaidika kikamilifu na hifadhi zetu za baharini, changamoto hizi lazima zitatuliwe," alisema Dkt. Rashid Ali Salim.

Naye kwa upande wake, Mratibu wa Mradi ambaye pia ni Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Tanzania (MPRU), Bw. Godfrey Ngupula, alieleza kuwa hali ya miamba ya matumbawe nchini bado ni nzuri, japokuwa katika miaka ya karibuni ilikumbwa na athari kubwa kutokana na uvuvi wa mabomu.

"Tuna jukumu la kulinda rasilimali zetu; kuharibu miamba ya matumbawe kunaweza kudhoofisha uchumi wa jamii za Pwani na mapato ya taifa ambayo kwa kiasi kikubwa yanategemea miamba ya matumbawe hivyo kuanzishwa kwa mpango huu wa kimkakati kutaimarisha ulinzi wa maeneo haya," alisema Bw. Ngupula.

Halikadhalika, Bw. Ngupula alieleza kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wavuvi wadogo katika maeneo ya Pwani wanategemea rasilimali kutoka kwenye miamba ya matumbawe, huku Tanzania ikikadiriwa kupata mapato ya takribani dola za Kimarekani bilioni 14 kutoka kwenye rasilimali hizo.




# MPRU YASHIRIKI SEMINA YA MKAKATI WA KITAIFA WA KUSIMAMIA NA KUENDELEZA MISITU YA MIKOKO

Na **Arafat Mnyau**

Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Tanzania (MPRU) imeshiriki uzinduzi wa Mkakati wa Kitaifa wa Kusimamia na Kuendeleza Misitu ya Mikoko ambapo mgeni rasmi alikuwa ni Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Balozi Pindi Chana katika Hoteli ya Protea iliyopo jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika uzinduzi huo uliofanyika Agosti 05, 2025, Mhe. Balozi Waziri Pindi Chana alisema Mikoko ni nyara ya Serikali inayotakiwa kulindwa kutokana na umuhimu wake kwa jamii na mazingira.

“Mikoko ni uti wa mgongo wa uhai wa Bahari ya Hindi. Huchuja taka, huzuia mmomonyoko wa fukwe, ni hifadhi ya kaboni, na ni mazalia ya samaki. Kuiacha iharibiwe ni kuhatarisha maisha ya watu na viumbe,” alisema Waziri Chana mbele ya viongozi wa serikali, wanadiplomasia na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa.

Waziri Chana alibainisha kuwa Tanzania ina zaidi ya hekta 158,100 za mikoko zinazosambaa katika wilaya 14 za ukanda wa Pwani. Hata hivyo, rasilimali hiyo imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo uvamizi wa maeneo, ujenzi holela, uchimbaji wa mchanga na uchafuzi wa mazingira.

Katika kukabiliana na changamoto hizo, Waziri Chana alisisitiza taasisi husika zichukue hatua mahsusi zifuatazo: Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kushirikiana na mamlaka nyingine katika kulinda na kusimamia mikoko; taasisi za utafiti kufanya tafiti zenye mweleko wa matumizi endelevu ya rasilimali hiyo; Wizara kushirikiana na sekta ya utalii kubadilisha mikoko kuwa vivutio vya kiutalii; na wadau wa maendeleo kuendelea kutoa msaada wa kifedha, kitaalamu na kiufundi ili kufanikisha utekelezaji wa mkakati huo kwa ufanisi.

Katika uzinduzi huo wa Mkakati huo, MPRU iliwakilishwa na Mhifadhi Mfawidhi kutoka Hifadhi ya Bahari ya Ghuba ya Mnazi na Maingiliano ya Mto Ruvuma (MBREMP) pamoja na Mhifadhi Mfawidhi, Maria Pentzel.





# MPRU YASHIRIKI MAONESHO YA KIMATAIFA YA BIASHARA YA 49 SABASABA 2025

Na **Arafat Mnyau**

Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Tanzania (MPRU) imeshiriki Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya 49 (Sabasaba) yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Sabasaba jijini Dar es Salaam, ikiwa ni jitihada za kuonyesha huduma mbalimbali zinazotolewa na Taasisi hiyo pamoja na kutoa elimu kwa wananchi.

Wawakilishi waliokuwepo kwenye Banda la MPRU waliongozwa na Afisa Masoko Halima Tosiri, Afisa Uhusiano Bw. Ivan Kimaro pamoja na wengine waliweza kutoa elimu kuhusiana na shughuli zinazofanywa na Taasisi ikiwemo Uhfadhi wa Bahari na utunzaji wa rasilimali zake kama vile mikoko, matumbawe na jinsi kulimo cha mwani kinavyoweza kuzalisha fursa za kibiashara kwa wajasiriamali na kuinua uchumi wa Mtanzania katika jitihada za kuinua Uchumi wa Buluu nchini.

Maonesho hayo ya Sabasaba ni



fursa ya kipekee kwa MPRU kuwasiliana moja kwa moja na wananchi na wadau mbalimbali wa Utalii hususan katika utalii wa Bahari ili kuboresha utoaji wa huduma na kuelimisha kuhusu umuhimu wa Uhifadhi wa Bahari katika kuendeleza na kukuza sera ya Uchumi wa Buluu nchini kwa pamoja.

# MPRU YASHIRIKI SEMINA YA KIMATAIFA YA MAENDELEO NA USIMAMIZI WA UCHUMI WA BAHARI NCHINI CHINA



Na **Arafat Mnyau**

Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Tanzania (MPRU) imeshiriki semina ya Kimataifa kuhusu Maenedeleo na Usimamizi wa Uchumi wa Bahari yaliyofanyika kuanzia tarehe Juni 11-26, 2025 katika Mji wa Xiamen, Mkoa wa Fujian nchini China.

Mafunzo hayo, yaliyoandaliwa na Fujian Institute of Oceanography (FJIO) kwa ufadhili wa Wizara ya Biashara ya China, yalileta pamoja wataalamu na watunga sera kutoka Bangladesh, Kenya, Malaysia, Mauritius, Nigeria na Tanzania, kwa lengo la kuimarisha maarifa na ushirikiano katika kukuza uchumi wa buluu duniani.

Bw. Bernard Ngatunga, aliyewakilisha Tanzania kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU), alijiunga na washiriki wengine kujadili mbinu endelevu za usimamizi wa rasilimali za bahari, ukuzaji wa ufugaji wa samaki (aquaculture), ubunifu katika bandari na teknolojia ya kibaolojia ya baharini.




Akizungumza katika semina hiyo, Bw. Ngatunga alisema semina hiyo imetoa mafunzo muhimu kuhusu namna ambavyo nchi zinazoendelea zinaweza kusawazisha maendeleo ya kiuchumi na uhifadhi wa mazingira.

“Mafanikio ya China katika upangaji wa matumizi ya bahari, usimamizi shirikishi wa Pwani na ukuzaji wa ufugaji wa samaki ni somo muhimu ambalo linaweza kuigwa katika mazingira ya Tanzania,” alisema Ngatunga.

Mafunzo hayo yameweka msisitizo mkubwa juu ya ushirikishwaji wa wadau, uratibu kati ya taasisi mbalimbali, na matumizi ya teknolojia za kisasa kama Geographic Information System (GIS) na picha za satelaiti kwa usimamizi bora wa rasilimali za bahari.




# MKUU WA WILAYA YA MTWARA AZINDUA RASMI TAMASHA LA NYANGUMI 2025

Na **Arafat Mnyau**

Mkuu wa Wilaya ya Mtwara Mhe. Abdallah Mwaipaya amewahimiza wananchi na wageni kutembelea vivutio mbalimbali vilivyopo katika Mkoa wa Mtwara, ikiwemo eneo la Msimbati ambko Nyangumi huonekana kwa wingi kuanzia Agosti hadi Novemba kila mwaka.

Mhe. Mwaipaya alitoa rai hiyo tarehe 17 Septemba 2025, wakati akizindua rasmi Tamasha la Msimu wa Nyangumi katika viwanja vya Mashujaa Park.

Akizungumza katika uzinduzi huo, alisema kuwa tamasha la mwaka huu ni fursa kubwa ya kuutangaza Mkoa wa Mtwara kupitia utalii wa bahari, vivutio vya asili na urithi wa utamaduni.

“Pamoja na mambo mengine, kupitia tamasha hili tutashuhudia michezo mbalimbali ikiwemo kuogelea, kuendesha mitumbwi na riadha. Michezo hiyo itafanyika katika fukwe za bahari za Mnazi Bay,



kuangalia milima ya mchanga, maingilio ya Mto Ruvuma kwenye Bahari ya Hindi, na kupumzika katika fukwe nzuri za Msimbati,” alisema Mhe. Mwaipaya.

**Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Abdallah Mwaipaya, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Patrick Sawala, aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kwenye viwanja vya** Mashujaa kujifunza na kujionea vivutio mbalimbali vinavyopatikana katika maonyesho hayo ikiwemo Simba na Tausi.

Tamasha la Nyangumi Festival linafanyika kuanzia Septemba 17 hadi 20, 2025, na kilele chake kitafanyika katika fukwe za Msimbati.




# TUSIHUJUMU VIUMBE WA BAHARINI KWA UVUVI HARAMU NA TAKA NGUMU-DC MTWARA

Na **Arafat Mnyau**

Mkuu wa Wilaya ya Mtwara Mhe. Abdallah Mwaipaaya ameeleza kuwa Tamasha la Nyangumi ni alama ya mshikamano kati ya Uhifadhi wa mazingira, maendeleo ya kiuchumi na urithi wa kitamaduni kwani Nyangumi si tu kivutio cha utalii, bali ni ishara ya maisha ya baharini na urithi wa kizazi cha sasa na kijacho.

Mhe. Mwaipaya alitoa kauli hiyo tarehe 20 Septemba 2025 akihitimisha Tamasha la Nyangumi lililofanyika fukwe za Msimbati.

“Tumeshuhudia wageni kutoka sehemu mbalimbali za Tanzania na nje ya nchi wakifika hapa Msimbati, Wajariamali wakishiriki katika maonesho ya sanaa, utamaduni na bidhaa. Hii inatupa fundisho kuwa uhifadhi na maendeleo haviwezi kutenganishwa. Tukiulinda urithi huu wa baharini, tunafungua milango ya ajira, mapato na maendeleo endelevu.” Alieleza Mhe. Mwaipaya.

Nyangumi huonekana Mtwara hasa katika Hifadhi ya Bahari ya Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma-Msimbati (MBREMP), kuanzia mwezi Agosti mpaka Novemba kila mwaka.





# WAHIFADHI BAHARI, WANAJAMII WA MAFIA WAHITIMISHA MAFUNZO YA UKUFUNZI WA UREJESHWAJI WA MATUMBAWE NCHINI INDONESIA

Na **Mwandishi Wetu**

Watumishi wa Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Tanania (MPRU) pamoja na Wanajamii wa Kisiwa cha Mafia wamemaliza mafunzo ya wiki nne (4) ya Urejeshwaji wa Miamba ya Matumbawe yaliyofanyika katika eneo la Raja Ampat nchini Indonesia.

Mafunzo haya yaliandaliwa na Shirika lisilo la Kiserikali la Ropes of Hope kwa lengo la kuongeza ujuzi wa kitaalamu na uwezo wa ukufunzi kwa washiriki kutoka Tanzania.

Katika kipindi cha mafunzo, washiriki walihusishwa moja kwa moja kwenye kazi za vitendo za kurejesha matumbawe, zikiwemo mbinu za upandaji, ufuatiliaji na usimamizi wa miamba ya bahari.

Matokeo ya moja kwa moja ni pamoja na usimikaji wa miundo ya kusaidia ukuaji wa matumbawe kama metal spiders, mesh na rope nursery, pamoja na upandaji wa zaidi ya vipande 700 vya matumbawe katika maeneo ya Sapokren, Davang na Yenbekwan. Vilevile, vitalu vya matumbawe (nurseries) vilianzishwa na kupandwa zaidi ya vipande 3,000 huku viumbe waharibifu wa miamba (crown-of-thorns starfish) 82 wakiondolewa ili kulinda afya ya matumbawe.

Akizungumzia mafunzo hayo, Mhifadhi Bahari wa MPRU, Pashcal Mkongola, alisema, kuwa wameweza kupata ujuzi wa wa kiteknolojia utakaowezesha kufanya kazi za urejeshwaji wa matumbawe kwa ufanisi zaidi.

"Ujuzi huu ni wa kipekee kwa Tanzania, tunaweza kutumia mbinu za kiteknolojia tulizojifunza kwa ufanisi zaidi katika urejeshwaji wa matumbawe na muhimu zaidi, tumepata uwezo wa kufundisha na kushirikisha wengine." alisema Bw. Paschal Mkongola.

Kwa upande wao, wanajamii waliowakilisha Mafia, Bw. Mikidadi Ahmadi na Bw. Hatibu Sheshe, walisema mafunzo hayo yamewapa mwamko mpya wa kushirikiana na jamii zao kulinda rasilimali za bahari.

"Tutatumia ujuzi huu kuelimisha na kushirikiana na wavuvi na wanajamii wenzetu kwa ajili ya maisha endelevu ya Pwani" alisema Bw. Mikidadi Ahmad.

MPRU inategemea kwa ujuzi walioupata washiriki utaleta manufaa makubwa katika kuendeleza juhudi za Uhifadhi na matumizi Endelevu ya Rasilimali za Bahari nchini. Kupitia nafasi yao ya sasa kama wakufunzi, washiriki hao watakuwa chachu ya mabadiliko kwa kuwajengea uwezo wataalamu wa Uhifadhi na jamii za Pwani, hivyo kuongeza wigo wa ushiriki na kuimarisha uwajibikaji wa pamoja katika kulinda mazingira ya baharini.




# WATANZANIA WAPATIWA FURSA YA KUJIFUNZA KIDIJITALI JUU YA UHIFADHI WA MATUMBAWE

Na **Mwandishi Wetu**

Watanzania wamepatiwa fursa ya kujifunza juu ya Uhifadhi wa Miamba ya Matumbawe kupitia usomaji wa kimtandao (kidijitali) katika Mkutano uliowakutanisha wadau mbalimbali kujadili Mustakabari wa Uhifadhi wa Matumbawe na Utekelezaji ambapo Tanzania ni moja ya nchi ambayo ina aina ya Matumbawe yanayopatikana katika Ukanda wa Magharaibi mwa Bahari lakini kwa ujumla katika nchi saba zinazitekeleza mradi huu wa Uokoaji wa Matumbawe.

Meneja wa Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Tanzania Bw. Davis Mpotwa akizungumza pembezoni mwa Mkutano huo uliofanyika Oktoba 08, 2025 katika Hoteli ya Peacock iliyopo jijini Dar es Salaam alisema Tanzania ni Moja ya nchi ambayo ina aina ya Matumbawe yanayopatikana katika Ukanda wa Magharibi mwa Bahari lakini kwa ujumla katika nchi saba zinazotekeleza mradi huu wa Uokoaji Matumbawe.

"Kikao cha leo kinalenga kutoa fursa kwa watanzania kujifunza juu ya uhifadhi wa matumbawe kupitia usomaji wa kimtandao unaweza kujisajili kupitia mtandao kwa kushare link kutoka taasisi mbalimbali za serikali na wataenda katika vyuo vyao na mashirika yao kuhakikisha kwamba kijana wakitanzania anapata fursa ya kusoma kozi za online zinazohusu matumbawe na jinsi gani ya kuhifadhi matumbawe na kutumia taaluma za kisayansi kuhakikisha matumbawe yanalindwa na kuhifadhiwa" Alisema Bw. Mpotwa.

Naye, Mtafiti na Mwalimu kutoka Chuo Kikuu Cha Killmo cha Sokoine Rose Kicheleri amesema mradi umewasidia kupata taarifa muhimu ambazo zitasidia sana kufanya maamuzi ya uhifadhi wa matumbawe pamoja na kuendeleza matumbawe nchini.

Amesema wamehusika katika tafiti mbalimbali na kupata taarifa ambazo ni nzuri na zote zinasaidia hasa tafiti za matishio na fursa ambazo zinatokana na Matumbawe hasa uelewa wa wadau kutoka ngazi tofauti kuhusu matumbawe, mfano matishio na fursa nyingi sana hizi zinaendana na uchimi wa Buluu kwa Tanzania Bara bado hazijaweza kuchukuliwa na wadau mablimbali lakini kwa Zanzibar fursa hizi zinachukuliwa kwa nguvu.

Kwa upande wake, Afisa Uvuvi Mkuu kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bi. Upendo Hamidu amesema kwamba wanaangalia ushiriki wa makundi maalumu hasa wanawake na vijana kwenye kusimamia Matumbawe hasa athari zinazotokana na mabadiliko ya tabia nchi lakini pia shughuli za tabia nchi zinazo haribu.

Amesema mazalia ya samaki yanasababisha kutupatia kiapato pamoja na ulonzi wabahari lakini chamgamoto zinaathiri wadau mbalimbali waliopo kwenye jamii.



# USAFI WA KISIWA CHA JAMBE KUFUNGUA MILANGO YA UTALII TACMP

Na **Arafat Mnyau**

Hifadhi ya Bahari ya Tanga Silikanti (TACMP) kwa kushirikiana na Kamati Ndogo ya Uhifadhi ya Sahare (VLC Sahare) imekamilisha zoezi la usafi katika Kisiwa cha Jambe, Tanga, likiwa na lengo la kufungua vivutio vya utalii na kulinda mazingira ya baharini.

Hatua hii inakuja kufuatia ziara iliyofanywa Agosti 25, 2025 na Kaimu Meneja wa Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Tanzania Bw. Davis Mpotwa kwa kutembelea Kisiwa cha Jambe akiwa ameambatana na watumishi wa TACMP akiwemo Bw. Mvungi, David Kabodo na Joyce Mziray ambapo ziara hiyo ililenga kuanzisha shughuli za Utalii katika Kisiwa cha Jambe.

Zoezi la usafi lilifanyika Agosti 30-31, 2025, likihusisha wanakamati 13 wa VLC Sahare na wakazi watatu wa eneo hilo. Takribani shilingi milioni 1.62 zilitumika kununua vifaa vya usafi, sare na posho za washiriki.



Mwenyekiti wa VLC Sahare, Bw. Jumaa Mbwana na timu yake ilifanikiwa kufungua njia vinjari katika maeneo ya kihistoria kama mnara wa enzi za ukoloni, visima na mashamba ya kale.

Aidha, Ripoti ya TACMP inaeleza kuwa eneo maalum limechaguliwa kwa ajili ya ujenzi wa mabanda ya utalii yanayoangalia Bahari ya Hindi na Jiji la Tanga. Hata hivo, changamoto ya upungufu wa kazi na utegemezi wa kazi za kujitolea imetajwa kuathiri ufanisi wa usafi huo.

TACMP imependekeza kufanyika kwa usafi wa nyongeza, kutafuta wawekezaji na kuweka alama za maelekezo kwenye njia vinjari, ili kuboresha zaidi mandhari ya kisiwa hicho chenye vivutio vya kiasili na kihistoria.

# MPRU WARSHA YA KUHUISHA MPANGO WA JUMLA WA UHIFADHI DMRS



Na **Mwandishi Wetu**

Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Tanzania (MPRU) imeongoza warsha ya siku mbili ya kupitia na kuhuisha Mpango wa Jumla wa Uhifadhi (General Management Plan – GMP) wa Dar es Salaam Marine Reserves System (DMRS), warsha iliyofanyika Disemba 20, 2025 katika ukumbi wa Makumbusho ya Taifa.

Warsha hiyo ilifunguliwa rasmi na Kaimu Meneja wa Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu, Bw. Davis Mpotwa, ambaye alisisitiza umuhimu wa kuwa na GMP iliyoimarishwa ili kukidhi mahitaji ya sasa ya uhifadhi wa bahari. Akizungumza wakati wa ufunguzi, alibainisha kuwa mabadiliko ya kimazingira, kijamii na kiuchumi yanahitaji mipango inayopimika na inayotekelezeka, hivyo kufanya mchakato wa mapitio kuwa hatua muhimu kwa kituo cha DMRS. Kwa kuzingatia hayo, warsha imewakutanisha wadau kutoka Taasisi za Kiserikali, Sekta Binafsi, Asasi zisizo za Kiserikali (NGOs), pamoja na watafiti na wataalamu wa masuala ya bahari. Kupitia majadiliano yao, wadau wamekuwa wakichambua maeneo muhimu ya GMP kwa lengo la kuoanisha mpango huo na hali halisi ya sasa ya kiikolojia na maendeleo ya jamii za Pwani.

Katika mazungumzo na wadau mbalimbali akiwemo Magreth Nkya, Mtendaji wa Kata ya Tungi (Kigamboni), amesema kuwa "Mapitio haya yataleta tija kubwa kwa sababu yameshirikisha wadau kuanzia hatua za awali. Wadau wa uhifadhi wa bahari wanafahamu changamoto hizi kwa karibu, hivyo ushirikishwaji huu utafanikisha nyenzo hii (GMP) na kuleta matokeo chanya kwa uchumi na jamii za pwani pamoja na taifa kwa ujumla."

Akiongeza kuhusu umuhimu wa ushirikiano, Fadhili Makwala, Makamu Mwenyekiti wa BMU, alisema: "Ushirikiano kati ya MPRU na BMU umeendelea kuboresha hali ya uhifadhi kwenye maeneo ya hifadhi. Ni muhimu kuimarisha ulinzi wa rasilimali za bahari kwa kufanya kazi pamoja, hasa katika kutoa elimu ya uhifadhi ili jamii iwe na uelewa mpana wa matumizi endelevu ya rasilimali hizo."

Warsha hii ni sehemu ya jitihada za jitihada endelevu za MPRU kuhakikisha kuwa usimamizi wa maeneo ya Baharini unaendana na mabadiliko ya mazingira, mahitaji ya jamii na dira ya taifa ya uhifadhi wa rasilimali za bahari

# WATUMISHI WATATU (3) MPRU-TMRS WAPATIWA MAFUNZO YA UREJESHWAJI WA MIAMBA YA MATUMBAWE



Na **Mwandishi Wetu**

Watumishi watatu (3) kutoka Hifadhi za kutoka Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Tanzania (MPRU) kituo cha Tanga Marine Reservation System (TMRS) wamefanikiwa kumaliza program ya mafunzo ya Urejeshaji wa Miamba ya Matumbawe (Coral Reef Restoration) yaliyofanyika kwa muda wa siku kumi kuanzia Septemba 1-10, 2025 katika fukwe iliyopo Jambiani, Zanzibar.

Mafunzo hayo yalishirikisha watumishi watatu (3) kutoka MPRU-TMRS akiwemo Bw. Jacob Edes, Bw. Emmanuel Madeni pamoja na Bw. Uchimbila ambapo waliweza kupatiwa ujuzi kuhusu Urejeshaji wa Miamba ya Matumbawe ikiwa ni hatua muhimu ya kuhakikisha ulinzi na ustawi wa viumbe hai wa baharini na usimamizi endelevu wa rasilimali zake.





Mafunzo hayo yalifadhiliwa na The East African Crude Oil Pipeline Project (EACOP) na kutekelezwa na Wildlife Conservation Society (WCS).



# MPRU NA WANAJAMII MAFIA WASHIRIKI MAFUNZO YA UREJESHWAJI WA MIAMBA YA MATUMBAWE NCHINI INDONESIA

Na **Mwandishi Wetu**

Shirika lisilo la Kiserikali la Ropes of Hope limewezesha mafunzo ya uhifadhi na urejeshwaji wa matumbawe yanayofanyika nchini Indonesia kwa muda wa wiki nne kuanzia Agosti 2025.

Mafunzo haya yamelenga Hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Mafia (MIMP) ambapo watumishi wa Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Tanzania (MPRU) pamoja na wanajamii kutoka Mafia wamepata nafasi ya kushiriki ili kuongeza ujuzi na kuutumia katika kuleta mabadiliko chanya kwenye juhudi za uhifadhi wa matumbawe nchini Tanzania.

Akizungumzia mafunzo hayo, Mhifadhi Bahari wa MPRU, Pascal Mkongola, alisema: “Mafunzo haya ni muhimu kwa taasisi na jamii kwa ujumla katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi. Kupitia mafunzo haya tunaweza kuimarisha juhudi za urejeshwaji wa matumbawe ambayo ni rasilimali muhimu kwa ustahimilivu wa mazingira ya baharini na maendeleo ya jamii za pwani.” Washiriki wengine kutoka Jibondo, Mafia ni pamoja na Mikidadi Ahmadi na Hatibu Sheshe, waliowakilisha wanajamii katika safari hii ya kujifunza na kubadilishana uzoefu.

Uhifadhi wa matumbawe una nafasi kubwa kwa jamii za pwani kwani hutoa makazi na mazalia ya samaki na viumbe wengine wa baharini, vinavyotegemewa kama chakula na chanzo cha kipato kupitia uvuvi endelevu. Aidha, miamba ya matumbawe hufanya kazi ya asili ya kulinda fukwe dhidi ya mmomonyoko unaosababishwa na mawimbi makubwa na dhoruba, hivyo kusaidia kulinda makazi ya watu, miundombinu na kuendeleza maisha ya pwani.

MPRU inaendeleza ushirikiano na taasisi ya Ropes of Hope katika elimu na shughuli za urejeshwaji wa matumbawe sambamba na kuimarisha ushirikiano na taasisi na mashirika mengine ya kitaifa na kimataifa. Ushirikiano huu unalenga kuongeza uelewa, kubadilishana maarifa na teknolojia, pamoja na kujenga uwezo wa pamoja katika kukabiliana na changamoto zinazotishia ustahimilivu wa mifumo ya ikolojia ya baharini kwa manufaa ya sasa na vizazi vijavyo.



# MPRU YAFIKIA WANANCHI KWA WINGI KATIKA MAONESHO YA NANENANE MKOANI LINDI

Na **Mwandishi Wetu**

Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Tanzania (MPRU) kupitia Hifadhi ya Bahari ya Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma (MBREMP) imeshiriki kikamilifu katika maonesho ya Nane Nane yaliyofanyika viwanja vya Ngongo, mkoani Lindi. Ushiriki huo ulilenga kutoa elimu na uhamasishaji kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa bahari na rasilimali zake kwa maendeleo endelevu ya jamii na taifa kwa ujumla.

Katika banda la MPRU, wananchi walipata elimu ya sera, sheria na kanuni za uvuvi, uvuvi endelevu wenye tija kwa jamii na mazingira, umuhimu wa utalii wa baharini na viumbe wake adimu kama vile nyangumi, samaki na viumbe wengine, lishe bora kupitia ulaji wa samaki, dagaa na mazao mengine ya baharini, madhara ya uvuvi usiokubalika pamoja na dhana za uvuvi halali.

Kupitia maonesho haya, zaidi ya 1,200 walitembelea banda la MPRU na kujifunza kuhusu fursa na manufaa yanayotokana na uhifadhi wa bahari. Vifaa mbalimbali vya kielimu ikiwemo mabango, flip charts na vielelezo vya viumbe vya baharini vilitumika kufikisha elimu kwa wananchi.

MPRU itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuhakikisha jamii zinaelimishwa kuhusu umuhimu wa rasilimali za bahari, ili kukuza uchumi wa buluu na kutunza mazingira kwa vizazi vya sasa na vijavyo.



# MPRU YAELEZA UMUHIMU WA UHIFADHI WA BAHARI KATIKA KUKUZA UCHUMI WA BULUU

Na **Mwandishi Wetu**

Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Tanzania (MPRU) imeshiriki kikamilifu katika Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo (Nane Nane) yaliyofanyika kuanzia Agosti 1–8, 2025 jijini Dodoma.

Kupitia maonesho haya, MPRU imeeleza juhudi zake katika kulinda na kuendeleza rasilimali muhimu ikiwemo matumbawe, nyasi bahari, mikoko, pamoja na ulinzi wa viumbe vya baharini na ikolojia ya bahari kwa ujumla.

Aidha, ilisisitiza mchango wa rasilimali hizo katika kukuza uchumi wa buluu na kutoa fursa za ajira na uwekezaji.

Akizungumza katika banda la MPRU, Afisa Masoko wa MPRU, Bi. Halima Tosiri, amebainisha vivutio mbalimbali vya utalii wa baharini vilivyo chini ya usimamizi wa MPRU, ambavyo vinajulikana kwa fukwe za kuvutia, michezo ya majini, na uwepo wa viumbe wakubwa wa baharini kama vile pomboo, papa potwe, nguva (Dugong) na nyangumi.

“Tunaelekea kwenye msimu wa nyangumi katika Hifadhi ya Bahari ya Maingilio ya Mto Ruvuma–Mnazi Bay. Tutakuwa na Tamasha Kubwa la Nyangumi litakalofanyika Mtwara mjini sambamba na safari maalumu za kuwaona nyangumi katika eneo la Mnazi Bay,” amesema Bi. Tosiri.

Kwa upande wake, Kaimu Meneja wa Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu, Bw. Davis Mpotwa, alisema kuwa MPRU inaendelea kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali wa uhifadhi ili kuhakikisha rasilimali za bahari zinalindwa na kunufaisha taifa kwa muda mrefu.

“MPRU inatekeleza mradi wa urejeshwaji wa matumbawe nchini kote. Hivi sasa tupo katika hatua ya kutoa elimu kwa jamii za pwani kuhusu umuhimu wa matumbawe ili kushiriki skikamilifu katika kuyahifadhi na kutunza rasilimali za bahari,” amesema Bw. Mpotwa.

Kwa ujumla, ushiriki wa MPRU katika maonesho ya Nane Nane 2025 umeendelea kuimarisha uelewa wa wananchi kuhusu nafasi ya uhifadhi wa bahari katika kukuza uchumi wa buluu na kuendeleza sekta ya utalii wa baharini nchini.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

HIFADHI ZA BAHARI NA MAENEO TENGEFU TANZANIA

## Tembelea Tovuti Kufahamu Shughuli za Utalii katika Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu

"Let's Us Share the Gift of Nature Together"


**IMEANDALIWA NA**

**ARAFAT MNYAU**
Mwandishi/Writer

**IVAN KIMARO**
Mhariri Mkuu/Chief Editer

**AILARS DAVID**
**HALIMA TOSIRI**
Wahariri Wasaidizi/Sub-Editors

**HELADIUS BAYINGANA**
**ABAS MAIGE**
Michoro & Usanifu/Graphics & Design